JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

04 **HISABATI**

Muda: Saa 2:00 **Jumatano, 06 Septemba 2017 asubuhi**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye maswali **hamsini (50).**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Soma maelekezo yote yaliyoko katika **karatasi maalum ya kujibia (OMR)** na kujaza taarifa zote.
4. Andika **namba yako ya mtihani** kisha **weka kivuli** kwenye tarakimu za namba hiyo mahali panapohusika kwenye karatasi yako ya kujibia.
5. Kokotoa kila swali na kisha **weka kivuli** kwenye herufi ya jibu lililo sahihi kwa kila swali katika karatasi yako ya kujibia uliyopewa, kwa mfano kama jibu sahihi ni A weka kivuli kama ifuatavyo:

[A]	[B]	[C]	[D]	[E]

6. Ukigundua kuwa herufi uliyoweka kivuli **si jibu sahihi** futa kivuli hicho kwa umakini kwa kutumia **kifutio safi** kabla ya kuweka kivuli katika herufi mpya.
7. Tumia penseli ya **HB** tu.
8. Simu za mkononi na vikokotozi **haviruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.

1 707004 100017

Scanned with CamScanner

SEHEMU A: MATENDO YA KIHISABATI

Katika swali la 1 – 25, kokotoa swali ulilopewa na kisha **weka kivuli kwenye herufi ya jibu lililo sahihi** katika karatasi yako ya kujibia.

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
1.	$68.9+57.5=$ A 116.3 B 125.4 C 126.4 D 115.3 E 126.3.	
2.	$8+73+109=$ A 189 B 192 C 173 D 190 E 187.	
3.	$856-378=$ A 378 B 466 C 477 D 478 E 485.	
4.	$472+8.939=$ A 8.301 B 8.311 C 9.311 D 9.301 E 9.411.	
5.	$1\frac{3}{8}+2\frac{1}{8}=$ A $3\frac{1}{2}$ B $3\frac{1}{4}$ C 4 D $3\frac{4}{16}$ E $\frac{7}{8}$.	
6.	$2\frac{4}{5}-1\frac{2}{5}=$ A $1\frac{1}{15}$ B $1\frac{2}{15}$ C $1\frac{2}{5}$ D $1\frac{2}{3}$ E $1\frac{4}{5}$.	

Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
7.	$-19+(3+^{-}11)=$ A 9 B 10 C 11 D $^{-}11$ E $^{-}10$.	
8.	$-13-(7-8)=$ A 13 B 14 C 2 D $^{-}2$ E 12.	
9.	$1\frac{3}{5}\div 1\frac{1}{4}=$ A $1\frac{7}{25}$ B $1\frac{17}{25}$ C $1\frac{3}{20}$ D $1\frac{3}{5}$ E $1\frac{3}{4}$.	
10.	$7.416\div 24=$ A 219 B 309 C 319 D 39 E 209.	
11.	$0.2\times 9.8=$ A 1.86 B 3.4 C 2.4 D 0.96 E 1.96.	
12.	Tafuta thamani ya x katika $x-3(12+10)=5$ A 46 B 24 C 25 D 71 E 70.	
13.	Kuna $\frac{1}{4}$ ngapi katika 36? A 9 B 40 C 32 D 124 E 144.	

Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
14.	Ikiwa $107 - M = 18$. Thamani ya M ni A 89 B 88 C 98 D 99 E 86.	
15.	Kipeuo cha pili cha $\frac{4}{9}$ ni . A $\frac{16}{81}$ B $\frac{2}{3}$ C $\frac{2}{9}$ D $\frac{4}{3}$ E 36.	
16.	Kigawo Kikubwa cha Shirika (K.K.S) cha 12, 18 na 24 ni A 2 B 3 C 4 D 6 E 8.	
17.	Badili $4\frac{1}{2}\%$ kuwa sehemu rahisi. A $\frac{9}{20}$ B $\frac{9}{200}$ C $\frac{45}{100}$ D $\frac{45}{10}$ E $\frac{45}{100}$.	
18.	Ikiwa $6x = -2$, tafuta thamani ya $\frac{6}{x}$. A -3 B -9 C -18 D -12 E -24.	
19.	Rahisisha $(6x)^2 \div 3x$ A $2x$ B $3x$ C $4x$ D $6x$ E $12x$.	
20.	Badili $\frac{1}{8}$ kuwa asilimia. A 8% B 12.5% C 24.5% D 25% E 50%.	



Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
21.	Mwanafunzi wa Darasa la Saba alikimbia umbali wa meta MCCLVIII kuzunguka uwanja wa mpira. Katika namba ya kawaida umbali huu ni sawa na A 1,158 B 1,208 C 1,257 D 1,258 E 1,273.	
22.	Meta 24 ni sehemu gani ya meta 36? A $\frac{2}{3}$ B $\frac{2}{9}$ C $\frac{1}{3}$ D $\frac{3}{2}$ E $\frac{1}{9}$.	
23.	Je, kuna namba tasa ngapi kati ya 13 na 19. A 1 B 2 C 3 D 4 E 5.	
24.	Badili $12\frac{1}{2}\%$ kuwa desimali. A 0.25 B 0.125 C 0.025 D 1.25 E 12.5.	
25.	Zidisha m7 sm30 kwa 5. Jibu liwe katika sentimeta. A sm 3,635 B sm 3,530 C sm 3.630 D sm 3,550 E sm 3,650.	




Scanned with CamScanner

SEHEMU B: MAUMBO




Katika swali la 26 – 38, kokotoa swali ulilopewa na kisha **weka kivuli kwenye herufi ya jibu lililo sahihi** katika karatasi yako ya kujibia.

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
26.	Tafuta eneo la mstatili ABCD, wenye mzingo wa sm 50.  A sm^2 136, B sm^2 126 C sm^2 146 D sm^2 156 E sm^2 225.	
27.	Tafuta mzingo wa msambamba ufuatao.  A sm 54 B sm 64 C sm 72 D sm 78 E sm 84 .	



Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
28.	Ben na Tina waligawana sawasawa kipande cha sabuni chenye ukubwa wa sm^3 252. Ikiwa kipande cha sabuni kilikuwa na urefu wa sm 42 na kimo sm 2 kama umbo linavyoonesha, tafuta upana wa kipande alichopata Ben.  A sm 1 B sm 2 C sm 3 D sm 4 E sm 5	
29.	Tafuta thamani ya x katika mchoro ufuatao:  A 10 B 15 C 20 D 30 E 45	
30.	Jina la umbo lifuatalo ni  A mstatili B mraba C pembetatu D duara E mistari minne.	



Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
31.	Tafuta thamani ya x katika umbo lifuatalo:  A 10° B 20° C 22° D 24° E 60° .	
32.	Andika majira ya nukta W katika grafu ifuatayo:  A (0, 4) B (-2, 4) C (-2, 0) D (4, -2) E (-2, -3)	
33.	Tafuta mzunguko wa duara lifuatalo ambalo kipenyo chake AB ni sm 200. (Tumia $\pi = 3.14$)  A sm 3.14 B sm 31.4 C sm 314 D sm 414 E sm 628.	


Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
34.	Eneo la pembetatu ABC ni sm^2 36. Je, eneo la pembetatu BCD ni sehemu gani ya eneo la pembetatu ABC?  A $\frac{1}{2}$ B $\frac{1}{3}$ C $\frac{2}{3}$ D $\frac{1}{4}$ E $\frac{1}{6}$.	
35.	Grafu ifuatayo inaonyesha alama alizopata Juma kwa miezi minne katika majaribio ya somo la Hisabati Muhula wa kwanza. Tafuta wastani wa alama hizo.  A 67 B 67.2 C 67.5 D 68 E 68.5.	

Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
36.	Tafuta ujazo wa umbo lifuatalo katika sm^3. (Tumia $\pi = \frac{22}{7}$)  A 660 B 1,320 C 3,520 D 4,620 E 4,720.	
37.	Tafuta jumla ya eneo la nyuso za mchemstatili ABCDEFGH wakati uso ABCD uko wazi.  A sm^2 3,200 B sm^2 3,000 C sm^2 1,200 D sm^2 2,200 E sm^2 10,200.	

Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
38.	Grafu kwa duara lifuatalo linaonesha michezo ambayo wanafunzi wa shule ya msingi Mwenge hupendelea kucheza. Ikiwa shule ina wanafunzi 400, je, wanafunzi wangapi wanapenda mpira wa miguu?  A 80 B 90 C 100 D 162 E 180.	

SEHEMU C: MAFUMBO

Katika swali la 39 – 50, kokotoa swali ulilopewa na kisha **weka kivuli kwenye herufi ya jibu lililo sahihi** katika karatasi yako ya kujibia.

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
39.	Gari-lilisafiri kwa mwendokasi wa kilomita 80 kwa saa kwa muda wa dakika 45. Tafuta umbali wa safari hiyo. A km 15 B km 30 C km 45 D km 60 E km 80.	

Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
40.	Teti alinunua vitu vifuatavyo sokoni; mchelele kilo 20 @ sh 1,200; Mayai 15 @ sh 250; kilo 5 za ngano @ sh 1,100; kilo 3 za nyama @ sh 6,500 na viungo mbalimbali kwa shilingi 2,800. Je, jumla alilipa shilingi ngapi? A 54,550 B 54,650 C 55,450 D 55,550 E 55,650.	
41.	Tupa alinunua redio kwa shilingi 450,000 na kisha kuiuza kwa shilingi 354,000. Je, Tupa alipata hasara ya shilingi ngapi? A 95,000 B 96,000 C 104,000 D 154,000 E 354,000.	
42.	Katungo alisafiri umbali wa km 3 kutoka Moshona kuelekea Magharibi hadi mji wa Katepo na kisha km 4 kuelekea Kusini hadi mji wa Kahenga. Endapo atakwenda Kahenga akitokea Moshona moja kwa moja bila kupitia Katepo, je atakuwa amesafiri kilomita ngapi? A km 3 B km 4 C km 5 D km 7 E km 12.	
43.	Mfanyabiashara alinunua mipira 20 kwa ajili ya kuuza dukani kwake. Ikiwa mipira 18 ilikuwa na ubora unaotakiwa na wateja, je ni asilimia ngapi ya mipira ilikuwa mibovu? A 2% B 20% C 18% D 38% E 10%.	
44.	Shule ya msingi Majengo ina wanafunzi 690. Ikiwa $\frac{2}{3}$ ya wanafunzi walifanya vizuri kwenye jaribio la Hisabati, je ni wanafunzi wangapi hawakufanya vizuri? A 230 B 330 C 450 D 460 E 660.	

Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
45.	Gharama ya kununua maembe mawili ya aina moja katika soko la Tegeta ni shilingi 2,000. Ikiwa Msafiri alinunua maembe matano ya aina hiyo, je, jumla alilipa shilingi ngapi? A sh 4,000 B sh 5,000 C sh 5,400 D sh 5,500 E sh 10,000.	
46.	Watoto wawili Natt na Pett waligawana Shilingi 18,000 katika uwiano wa 2:3 kwa mfululizo huo. Je, Pett alipata shilingi ngapi? A sh 3,600 B sh 7,000 C sh 7,200 D sh 10,500 E sh 10,800.	
47.	Shule ya msingi Maendeleo ilipanda miche ya miti 104 katika shamba la shule. Ikiwa $\frac{1}{4}$ ya miti ilikauka, je, ni idadi gani ya miti ilikauka? A 21 B 24 C 26 D 52 E 78.	
48.	Mashine ya kurudufu hutoa nakala 20 za karatasi kwa sekunde 40. Je, katika saa moja itarudufu nakala ngapi? A 60 B 90 C 800 D 1,200 E 1,800.	
49.	Mokiwa alikula $\frac{3}{10}$ ya mkate na Jenita alikula mkate huo mara mbili zaidi ya Mokiwa. Je wote pamoja walikula sehemu gani ya mkate? A $\frac{5}{10}$ B $\frac{9}{10}$ C $\frac{6}{10}$ D $\frac{2}{10}$ E $\frac{1}{10}$.	

Scanned with CamScanner

NA	SWALI	SEHEMU YA KAZI
50.	Wastani wa mapato ya muuza matunda kwa siku nne za wiki ni shilingi 20,000. Ikiwa mapato ya siku ya kwanza ni 22,000, siku ya pili ni 18,000 na siku ya tatu ni 16,000, je siku ya nne hupata shilingi ngapi? A 12,000 B 15,000 C 20,000 D 22,000 E 24,000.	

Scanned with CamScanner